# MWONGOZO WA TAMTHILIA TATU

- **MFALME EDIPODE**
- **KIMYA KIMYA KIMYA**
- **CHEMA CHAJIUZA**

## WAHAKIKI WA TAMTHILIA HIZI


- **EDWIN ARIIHO**
- **SIMON T KAWAIDA**


**2019**

**TAMTHILIA: MFALME EDIPODE**

**MWANDISHI: SOFOKILE**

**MWAKA: 1969**

**MFASIRI: SAMUEL S. MUSHI**

**Utamgulizi:**

Mchezo huu wa mfalme edipode uliandikwa na sofokile na kuchapishwa mara ya kwanza mwakani (1969). Lakini imekisiwa kuwa ulitungwa kati ya mwaka 429 na mwaka 420 kabla kristo, na ni mopjawapo wa mfululizo wa hadithi zinazohusiana na ufalme wa Thebe huko Ugiriki.

Mchezo huu ulitafsiriwa katika lugha ya Kiswahili na Samuel S. Mushin a umetoa mchango mkubwa katika fasihi ya Kiswahili. Ni mchezo wa aina yake wenye muundo wa kishairi na ambao haupangwi kwa maonyesho na vitendo kama ilivyo katika michezo mingine. Yote yaliyomo hutendeka maskani mwa mfalmeEdipode.

**Uchambuzi wa kichwa cha mchezo:**

Kichwa cha mchezo huu ni "Mfalme Edipode". Mfalme maana yake ni mtawala mwanamume aliyepata nguvu za utawala kwa njia ya urithi au uwezo mwingine kama vile ushujaa. Edipode kulingana na mchezo huu, humaanisha 'miguu iliyovimba'. Kwa hivyo, mchezo huu ukapewa kichwa hicho kulingana na yaliyo mtukia Edipode kwanzia pale anapofungwa miguu mpaka ikapata uvimbe, kupelekwa koronto na kurudi kwake ugiriki. Kwa kifupi, unayazunguka maisha yake Edipode tangu utotoni mpaka laana yake inapomfika na kufunuliwa kwake mpaka ikasababisha utoboaji wa macho yake kwa mikono yake mwenyewe.

**Uchambuzi wa picha ya jalada:**

Jalada la mchezo huu wa mfalme Edipode huonyesha kichwa cha mfalme ambacho kimechorwa kwa rangi nyekundu. Kichwa chenyewe kimetobolewa macho. Kulingana na yaliyomo, picha hii ya jalada huelezea giza analoliishi mfalme edipode kwa kufurahia ndoa na mwili wa mamake bila kujua, kitendo ambacho kinamfanya yeye kujitoboa macho yote mawili kwa kutumia vifungo vya vazi lake dhahabu, ili macho yake yasione tena aibu yake baada ya ukweli kufunuliwa kuwa ndiye najisi muuaji wa Laio babake mfalme wa Thebe na mwoaji wa mama mzazi kama ilivyotabiriwa na Apolo huko Delfi.

**Dhamira ya mwandishi/Mtunzi:**

Sofokile alidhamiria kuonyesha kuwa la mungu ni la mungu, haliwezi kuepukanwa. Kupitia tamthilia hii, anaonyesha utabiri kuwa mtoto atazaliwa katika nyimba ya mfalme na kuwa mtoto huyo huyo, atamuua babake na amwoe mamake mzazi. Lakini wazazi wa kitoto hicho baada ya kukizaa, wakahofu kukiua kwa mikono yao na kukipa mchunga wanyama akipeleke msituni huko kitaroni na akitupe huko. Kwa nguvu za mungu, mchunga wanyama naye vile akakihurumia kitoto na kukipa mchunga mwenzie akipeleke ugaibuni kikulie huko kisije kikarudi ugiriki. Huko alikopelekwa, katiwa kwenye ufalme wa korinto, nguvu ya mungu bado ingali. Mtoto kakuzwa kama mfalme mpaka anaposikia habari kutoka kwa m mpita njia mlevi kuwa polibo na merope hawakuwa wazazi wake edipode. Kwa wasiwasi, edipode kawaendea polibo na merope kuwauliza juu ya yale aliyoyasikia na wao wakamdanganya kuwa ndio wazazi wake halisi. Edipode kaenda kuuliza kwa miungu, na habari alizopata zikamshutua. Habari zenyewe zikawa zinasema kuwa alizaliwa na laana ya kumuua babake na kumwoa mamake. Kwa hofu nyingi, akakimbia kwao ili aje aepukane na msiba huo huo. Na kukimbilia ugiriki akidhani amekimbia nyumbani bila kujua alikokimbilia ndiko palikuwa nyumbani. Na mwishowe akamua babake na kumwoa mamake na kuzaa naye wana wawili na mabinti wawili. Kma ilivyotabiriwa, vikatukia na mji wa Thebe kuanza kuambukizwa na maradhi ya tauni na majonzi yakajaa ufalme wote.

**Ploti ya mchezo:**

Mchezo huu unaanzia maskani kwa mfalme Edipode na mkewe Jokasta ambapo kunakuja umati mkubwa wa raia wa Thebe na kukaa kama wahitaji. Edipode anakuja na kufika walipo na kuwaomba wamwambie linalowaudhi…..(uk 1). Raia wakiongozwa na Kahini, wanamwelezea linalowakefyakefya kuwa ni mkondo wa mauti yasiyoepukwa kwanzia rutuba, malisho ya wanyama, tumbo la uzazi na maradhi yaliyo maambukizi……(uk 2). Baada ya maneno yake yote kahini, Edipode anawaonyesha kuwa anawasitikia na kuwa ashaanza mipamgo ya kutambua chanzo cha hayo yote. Anawaelezea kuwa amemtuma kreoni kwa Apolo apate kuchunguza nini ni sababu ya kuambukizwa kunakoizingia mji wa Thebe……… (uk 4). Kreoni anaingia huku akitabasamuna kuwaelezea yaliyotoka kwa Apolo kuwa chanzo cha yote ni maluuni muuaji wa Laio, na kuwa kunatakiwa atafutwe na afukuzwe ufalmeni. Edipode anaapa kuwa ataanza kufichua siri ya kifo cha mfalme Laio……(uk 7). Anaingia ndani na jamii ya wazee wa Thebe wanaosema kwa kupokezana wanaingia huku wakiwaomba miungu wawaondolee maambukizi wote kwa utatu wao. Baada ya muda Fulani, Edipode anaingia na kusimama mbele ya wahitaji na kuanza kuwauliza ikiwa miongoni mwao kuna anayejua kuwa alihusika na kifo cha mfalme Laio. Kila mtu yu kimya…..(uk 13). Teresia anafika na kuwambia kuwa hatasema kitu na kumwambia Edipode asafishe nyumba yake.

Lakini kutokana na mvutano wea maneno kati yake Edipode na Teresia, Teresia anaishia kusema kuwa Edipode ndiye najisi……(uk 15). Akaendelea kumwambia kuwa “siku ya leo itakufunulia kuzaliwa kwako na ajali pia…….” (uk 19). Wanaondoka na kunabaki wazee wakijiuliza maneno kwa kupokezana .harafu, anaingia kreoni na kuvutana na Edipode kwa maneno huku wazee wakiwatuliza pamoja na Jokasta, mpaka kreoni anapotoka….(uk 27). Edipode anamwuliza Jokasta juu ya kifo cha mmewe Laio, na Jokasta anamwambia yote yaliyofika mmewe, na kuwa kuna mtumishi aliyewambia kuwa Laio aliuawa na msafiri huko njia panda. Edipode kwa hofu anamwagiza Jokasta kumwita huyo mtumishi mchunga wanyama….(uk 32). Hapo ndipo Edipode anapowambia Jokasta na wazee yanayomhusu toka korinto kwa nyumba ya polibo na mkewe Merope, mpaka kufika kwake Thebe Ugiriki. Wazee waonyesha kutishwa na yaliyosemwa na Edipode….(uk 35). Hapo ndipo mjumbe kutoka korinto anapoingia huku akiuliwa kwa Edipode. Wazee wanamwambia kuwa ndipo hapa….(uk 38). Habari anazowaletea akina Edipode ni kuwa babake mfalme polibo alifariki na kuwa umma wataka kumpa ufalme Edipode. Mambo yaendelea kuwachanganya wazee, Edipode na Jokasta. Lakini mjumbe kutoka korinto anawafafanulia kuwa Edipode hakuwa mwana wao polibo na merope, na kwamba kalelewa tu pale na ushahidi unaletwa na mchunga wanyama aliyemkabidhi kitoto(Edipode) kwa hofu klukiacha kiangamie huko kitaroni kama alivyoagizwa na mfalme Laio na malkia Jokasta. Baada ya Edipode kujua kuwa alimwua babake na kumwoa mamake, Jokasta anatoka na kujifungia chumbani huku akilia na kujinyonga. Naye vile Edipode aingia chumbani na kukuta mkewe akininginia ukambani na kumtoa na kutumia vifungo vya vazi lake kujitoboa macho kwa kuvipigilia macho vifungo hivyo ili yasije tena kuona aibu yake…..(uk 51). Edipode sasa yaingia akliwa kipofu huku akilaani aliyemsaidia alipokuwa amefungwa miguu, akisema, “kufa wakati huo Baraka yangu”….(uk 54). Akaomba atolewe nje ya mji wa Thebe. Kreoni anaingia. Edipode anamwomba kuwantunza vizuri wana wake na mabinti zake wapendwa Ismene na Antigone. Akamsihi kumzika jokasta na kumwomba kumtoa nje mbali na mji wa Thebe, huku akijutia kuzaliwa kwake. Mwishoni mwa mchezo, wazee, baada ya edipode kupelekwa ndani ya nyumba na kreoni ili waanze kupata maamuzi ya mungu, wanaanza tena kusema kwa kupokezana, wakilinganisha uwezo aliokuwa nao Edipode na msiba uliomwangukia. Wakisema……..

Kwa hiyo jueni kila mtu yampasa

Klutazamia hatima ya maisha yake

Na hakuna yeyote awezaye kuitwa

Mwenye furaha hadi siku ile ambayo

Atakwenda nayo kaburini kwa amani

**MAUDHUI YALIYOMO:**

Ni mambo muhimu yanayoelezwa kama vile katika hadithi, mchezo, hotuba au makala. Kwa mujibu wa mchezo huu, maudhui na mambo muhimu au makuu ambayo mtunzi Sofokile anayaeleza kupitia maandishi yake. Na ni kama yafuatayo:

- Utabiri
- Huruma
- Ndoa
- Vifo
- Safari
- Malezi
- Uongozi
- Malalamishi
- Utumikiaji
- Soni/haya/aibu
- Heshima
- Woga
- Majuto
- Hasira
- Uchungaji
- Maradhi
- Utamaduni
- Laana

**Utabiri:**ni jinsi au namna ya kubashiri mambo yatakayotokea. Katika mchezo huu, kuna utabiri kutoka kwa Apolo kuwa motto atazaliwa katika jumba la mfalme Laio na atamwua babake na amwoe mama mzazi. Na kulingana na yaliyomo, tunaona utabiri huu ukitukia kutokana na ufunuaji wa siri ya maambukizi yaliyouzingira na kuangamiza mji wa Thebe.

**Huruma:** humaanisha moyo wa wema. Kulingana na yaliyomo mchezoni, mchunga wanyama anakihurumia kitoto (Edipode) baada ya kutiwa mikononi mwake na mfalme Laio pamoja na malkia Jokasta ili akitupe huko kichakani kitaroni. Anakihurumia na kukipa mchunga wanyama mwenzie akipeleke koronto kikakulie huko ili kisije kikaleta maangamizi kama utabiri ulivyosema.

Huruma nyingine ni zake Edipode baada ya kufunuliwa siri za kuzaliwa kwake, anawahurumia mabinti zake Ismene na Antigone akimwomba kreoni mjomba wao ili awatunze watoto wake wasione tabu…..(uk 59).

**Ndoa:**ni makubaliano rasmi ya mwanamke na mwanamume kuishi pamoja kama mume na mke. Na mara nyingi ndoa husababisha kuzaliwa kwa watoto na hujaa mapenzi tele. Katika mchezo huu, kuna ndoa kati ya mfalme Edipode na malkia Jokasta inayopelekea kuzaliwa kwa wana wawili na mabinti wawili.

**Vifo:** kifo ni tukio au tendo la kufikia mwisho wa uhai. Katika mchezo huu, kuna vifo mbalimbali. Kwanza kabisa, kuna kifo cha mfalme Laio kinachosababishwa na mkono wa mwanawe Edipode kama ilivyotabiriwa na Apolo.

Pia, kuna kifo cha mfalme Polibo huko Korinto ambako Edipode alilelewa. Vile vile kuna vifo vya watumishi waliotembea na mfalme Laio ambao waliuawan msafiri huko njia panda nchini Foki.

Kuna kifo cha malkia Jokasta kinachosababishwa na mikono yake mwenyewe kwa kuhofu aibu ya kuzaa watoto na mwanawe halisi, baada ya kufunuliwa siri za chanzo cha maambukizi yaliyouzingira mji wa Thebe na kusababisha maafa mengi. ….(uk 50)

**Safari:**ni tendo la kwenda mahali Fulani ambapo ni mbali na pale mtu alipo. Katika mchezo huu, kuna safari yake Edipode kutoka korinto kwenda Ugiriki. Kuna safari yake mfalme Laio kutoka Ugiriki kwenda Foki. Pia kuna safari yake mjumbe kutoka korinto kwenda Ugiriki huko thebe kumtafuta Edipode ili arudi kwao korinto na aurithi ufalme wa Polibo.

**Malezi:**ni njia ya ukuzaji wa mtoto kwa kutarajiwa kufuata tabia na mwenendo unaostahiki. Katika mchezo huu, kuna malezi anayopewa Edipode kutoka kwa wazazi wake wa kambo akina Polibo na Merope. Malezi mengine yaliyomo ni ya Jokasta na mmewe wanayowapa wana wao na hasa mabinti zao.

**Uongozi:**ni madaraka anayopewa mtu ya kusimamia shughuli au asasi. Katika mchezo huu kuna uongozi wa kifalme ambapo tuna mfalme Edipode kama kiongozi wa ufalme wa Thebe huko ugiriki. Kuna mfalme Polibo kam kiongozi wa ufalme huko korinto. Pia kuna mfalme Laio aliyeuawa na mwanwe Edipode kama kiongozi wa ufalme wa Thebe kabla kuja kwake Edipode.

**Malalamishi:**ni maelezo yaonyeshayo kutoridhika na jambo Fulani au yaliyofanywa. Kulingana na mchezo huu wa mfalme Edipode, kuna kundi ra raia wa Thebe wanaolalamikia maambukizi yanayoawfika huku wakiongozwa na kahini. Wanamlalamikia mfalme wao Edipode huku wakimwomba usaidizi ili awaondolee m,auti yanayowasimanga.

**Utumikiaji:**ni hali ya kutenda kazi ya kuajiriwa kwa mujibu wa kanuni zilizowekwa. Kulingana na mchezo huu wa mfalme Edipode, kuna utumikiaji ambapo tunaona watumishi katika jumba la mfalme Edipode wakimtumikia malkia Jokasta na Edipode. Pia tunaona mjumbe kutoka korinto akitumikia jumba la mfalme Polibo na mkewe malkia Merope.

**Soni/Haya/Aibu:**ni jambo livunjialo mtu heshima. Kulingana na mchezo huu, kuna aibu kwa wahusika mbalimbali. Kwanza, kuna aibu kwa mfalme Edipode baada ya kufunuliwa siri za kuzaliwa kwake na kuwa ndiye najisi mwuuaji wa kipenzi mfalme Laio aliyerithi mkewe/ mamake malkia Jokasta. Jambo hili linapelekea kujitoboa macho kwake Edipode. Pili, kuna aibu kwa malkia Jokasta baada ya kugundua kuwa mtu aliyekuwa akifurahi naye kimapenzi kawa mwanake wa damu. Na kwa hivyo anaamua kujinyonga.

**Heshima:**ni thamaniya utu. Katika mchezo huu, tunaona raia wa Thebe wakimheshimu mfalme Edipode kwa kumtaja kama "habibi mkuu, mfalme wangu"__maneno yake kahini akiwasilisha yaliyowaleta yeye na raia wengine kwa mfalme Edipode…..(uk 2). Pia, tunaona Jokasta malkia wa ufalme akimheshimu bwana wake…..(uk 31)

**Woga:**ni hali ya kuwa na hofu ya kufikwa na jambo la kutisha au la tabu. Au, hali ya kutoweza kustahimili vitisho. Kulingana na mchezo huu, woga unabainika pale mfalme Laio na mkewe malkia Jokasta baada ya utabiri wa Apolo kuwa mwanao atamwua baba na amwoe mama. Kwa woga wa kitendo hicho kuwafika, wanaamua wakiue kitoto chao kichanga. Vile vile, kuna woga unaowafika pale wanaposhindwa kukiua kile kitoto kwa mikono yao ili wasije wakapata laana, na kuamua kukipa mchunga wanyama akitupe kitaroni.

Vile vile, woga unamshika Edipode baada ya kusikia utabiri kuwa atamwua baba na amwoe mama, na anaamua kutoroka korinto ili asije akamua Polibo na kumwoa Merope akidhani kuwa ndio wazazi wake halisi.

**Majuto**: ni huzuni inayosababishwa na kosa lililotokea. Kulingana na jinsi ilivyo mchezoni, kuna majuto ya Edipode baada ya kufunuliwa siri kuwa yeye ndiye chanzo cha mateso, anajutia kunusurika kwake kwa kifo babake na mamake walichokuwa wamempangia. Tunamwona akijutia kila kitu…………………

Ee mwanga! Laity nisikuone tena,

Kwa kuwa wazi nimekwishaonekana,

Mwenye dhambi katika kuzaliwa kwangu,

Tena mwenye dhambi katika ndoa yangu

Na mwenye dhambi kwa kumwua baba yangu!.........(uk 48)

**SIFA ZA WAHUSIKA:**

Wahusika ni viumbe wa kisanaa wanaotumiwa na mwandishi au mtunzi kuwasilisha ujumbe wake. Katika mchezo huu wa mfalme Edipode kuna wahusika wafuatao pamoja na sifa zao:

**Edipode:**ni mwanao mfalme Laio na malkia Jokasta na kwa upande mwingine ni mmewe malkia Jokasta na baba yao Ismene na Antigone.

- ✓ Ni kiongozi mtawala wa ufalme wa Thebe kwa kuwa tunamwona akisimama kama mfalme na kupewa heshima na raia wa ufalme wote wa Thebe.
- ✓ Ni shujaa kwa kuwa anamshinda mwanamke aliyetia foara kuwanyanyasa na kwafanya watu wa Thebe watumwa kwa makafara baada ya kifo cha mfalme Laio .anawaokoa watu wa Thebe kotoka mikononi mwake.
- ✓ Ni mwenye hekima kwa kuwa anajibu mafumbo ya mwanamke aliyetia for a kuwaangamiza wakazi wa Thebe na kuwafanya watumwa kwa makafara.
- ✓ Ni mwenye mapenzi. Mapenzi yake kwa mkewe Jokasta na wanawe pamoja na mabinti zake. Anawaonyesha mapenzi mpaka ile saa ya mwisho wa furaha yake. Mapenzi yake kwa familia yake yanabainika pale anapowaachia kreoni awatunze wana wake na mabinti zake.
- ✓ Ni mwenye huruma. Kwa kuwa anawahurumia watu wa Thebe kwa sababu ya maambukizi yanayowazingira na kujaribu kutafuta chanzo cha maambukizi hayo pamoja na suluhisho.
- ✓ Ni najisi kwa kuwa anamwua babake mfalme Laio kwa kutojua huko nchini Foki kwenye njia panda moja ikielekea Delfi.
- ✓ Ni mwenye laana ya kumwua babake na kumwoa mamake kama utabiri wake Apolo ulivyosema.
- ✓ Ni mwenye hasira na hasira zake zinapatikan pale anapomfokea Teresia kwa maneno makali baada ya kuambia kuwa yeye ndiye chanzo cha kila teso lipatikanalo mjini Thebe.
- ✓ Ni mwenye aibu/soni,haya.

**Jokasta:** ni mkewe mfalme Laio na mkewe mfalme Edipode baada ya kifo cha Laio na kurithiwa na Edipode. Ni mama yao Edipode, wana wawili na Ismene na Antigone. Ni dada yake kreoni na pia malkia wa ufalme wa Thebe.

- ✓ Ni mwenye heshima kwa mmewe mfalme Edipode

- ✓ Ni mwoga na woga wake unabainika pale anapoamua yeye na mfalme Laio kukiua kitoto chao kichanga ili kisije kikamwoa yeye baada ya kumwua baba.
- ✓ Ni mpole na upole wake unapatikana pale anapojaribu kumtuliza moyo mme wake Edipode kuachana matusi kati yake na kreoni.
- ✓ Ni mwenye mapenzi kwa mmewe Edipode.
- ✓ Ni mwenye aibu kwa kuwa anajinyoga baada ya kufichuliwa kwa siri kuwa Edipode mmewe ni mwana wake halisi. Aibu inamfanya ajinyonge.

**Kreoni:**ni kaka yake Jokasta na mjomba wao Ismene na Antogone. Ni mkwewe Edipode na Laio.

- ✓ Ni mpole. Na upole wake uanapatikana pale anapofokewa na Edipode baada ya kuletwa kwa Teresia. Anamjibu kwa upole ingawa yeye Edipode anamfokea.
- ✓ Ni mwenye huruma kwa kuwa anamhurumia Edipode baada ya kujitoboa macho huklu akiomba kuwashika mabinti zake mikonono. Tunamwona anawamletea.
- ✓ Ni mtu mwenye kukubali kazi. Kwanza anakubali kazi ya kwenda kwa Foibo mkuu kuuliza chanzo cha mateso yanayowakabili raia wa Thebe. Pia, anakubali kazi ya kuwatunza na kuwalea wana wake Edipode hasa mabinti zake Ismene na Antigone…(uk 59)

**Teresia**: ni mtabiri kipofu mwenye uwezo wa kuona kile binadamu wa kawaida hawezi kuona. Ni mzungumzaji na miungu yaani anauwezo wa kuzungumza na mungu jambo ambalo haliwezekani kwa watu wakawaida. Anaonea mbali mambo kabla hajaambiwa. Na ni mficha siri.

- ✓ Ni mwenye hasira na hasira zake zinapatikana pale anapoamua kusema aliyokataa kusema mwanzoni baada ya kusimangwa na mfalme Edipode huku akimtwanga maswali.

**Kahini:**ni mmoja wao raia wa Thebe wanaolalamikia mfalme Edipode ili awaondolee mateso yanayowazingira.

- ✓ Ni msemaji kwa niaba ya raia wengine anayeteuliwa na mfalme Edipode kuwasilisha yanayowaudhi raia wa Thebe.
- ✓ Ni mwenye umri mkubwa na ndio sababu anateuliwa nas mfalme Edipode ili awasilishe yanayokefyakefya raia wote.
- ✓ Ni mwenye kuheshimu. Anamheshimu mfalme wao Edipode kulingana na maneno anayotaja mwanzoni mwa hotuba yake…….(uk 2)

**Mjumbe**: mtumishi katika ufalme wa korinto huko kwa mfalme Polibo na mkewe malkia Merope.

- ✓ Ni mwenye huruma kuwa kuwaalihurumia kitoto(Edipode) baada ya kukipokea kutoka mikononi mwa mchunga wanyama na kukipeleka ka Polibo kilipopatia maisha bora.
- ✓ Ni mchungaji kwa kuwa anakutana na wachunga wanyama wengine huko kitaroni kulingana na misimu mbalimbali.

**Mchunga:** analisha wanyama wa mfalme Laio na mkewe malkia Jokasta.

- ✓ Ni mwenye huruma kwa kuwa anakihurumia kitoto baada ya kukipokea mikononi mwa wazazi wenye nia ya kukiangamiza. Kwa huruma zake, anakiweka mikononi mwa mchungaji kutoka korinto ili akipeleke mbali na kwao.
- ✓ Ni mwoga. Woga wake unapatikana pale anapotwangwa maswali na Edipode akitaka kujua asili yake. Na kwa woga, anamwambia yote yanayomhusu ambayo alifyatia ulimi miaka mingi.
- ✓ Ni mficha siri. Ufichaji siri wake unapatikana pale anapofyata ulimi baada ya kutoka huko kataroni alikodhaniwa alikitupa kile kitoto. Vile, baada ya Edipode kupewa uongozi pale Thebe, anaamua kutoka ufalmeni akaenda kijijini kuchunga wanyama ili afiche siri yake vizuri.

**Mtumishi na watumishi**: wanatumikia jumba la mfalme Edipode na mkewe malkia Jokasta.

**Wazee:** jamii ya wazee wa Thebe wanaosema wote kwa pamoja na kupokezana.

- ✓ Ni wenye upole. Upole wao unabainika pale wanapowatuliza nyoyo akina Edipode na Kreoni baada ya Teresia kufichua mambo yanayohusiana na kifo cha mfalme Laio.
- ✓ Ni waombelezi kwa kuwa wanaonekana wakimwomba mungupamoja na miungu wao wote katika utatu wao, ili waje na wakawaondolee kuteswa na huzuni na maafa yanayowazingira.
- ✓ Ni wenye hekima. Maneno wanayoyasema mwishoni mwa mchezo huu yenye kufundisha na yenye ujumbe mzito.
- ✓ Ni washikaji wa imani pamoja na washikaji utamaduni.
- ✓ Ni wazee wenye umri mkubwa.

**Ismene na Antigone**: wanao mfalme Edipode na mkewe malkia Jokasta.

- ✓ Ni wenye huruma. Wanamhurumia na kumlilia baba yao kwa yote yanayomfika.
- ✓ Ni watoto wa dhambi waliozaliwa kutokana na ndoa ya dhambi iliyolaaniwa. Ni watoto wa kaka yao.

**Raia wa Thebe**: ni wakazi wa ufalme wa Thebe, wenye kufikwa maambukizi ya maradhi, maafa, mateso na huzuni kutokana na laana aliyopata mfalme wao Edipode kabla hajazaliwa.

<u>**MBINU ZA UTUNZI**</u>:

Hizi ni njia mbalimbali mwandishi/mtunzi anazotumia kuiunda kazi yake ili ujumbe anaolenga uwafike walengwa wake. Au, ni vipengele vinavyotumiwa na mwandishi kuwasilisha ujumbe wake. Na kulingana na mchezo huu wa mfalme Edipode, Sofokile alitumia mbinu zifuatazo:

**Ushairi**: hii ni sanaa ya utunzi wa mashairi. Kwanzia mwanzo wa mchezo huu mpaka mwisho wake, mwandishi ametumia ushairi huku akifuatia usawa wa mizani. Hasa pale wazee wanapozungumza kwa kupokezana.

**Mazungumzo**: ni hali ya kusema kwa watu wanaohusika kwa zamu. Mmoja anasema huku mwenzake akisikiliza na baadaye, anampa nafasi naye kusema huku akisikiliza. Katika mchezo huu, mwandishi ametumia hii mbinu kwanzia mwanzo hadi mwisho wake. Kwa mfano, Edipode anazungumza huku kahini na raia wengine wanasikiliza. Na baada yake, kahini anazungumza huku Edipode na raia wengine wakisikiliza.

**Taswira:** mbinu hii hujihusisha na ujenzi wa mawazo au picha akilini mwa msomaji kuhusu kile kinachoendelea mchezoni. Kwa mfano mtoto kuzaliwa na laana ya kumwua babake na kumwoa mamake hujenga hiyo picha ya jambo hilo kutokea akilini mwa msomaji.

**Majazi**: mbinu hii huhusika na kumpa mhusika jina kulingana na sifa au tabia na matendo yake. Katika mchezo huu, mwandishi amemchora Edipode na jina lake lenye kumaanisha miguu iliyovimba kutokana na yaliyomfita alipokuwa bado kitoto kichanga.

Pia, watumishi na mjumbe wamepewa majina hayo kulingana na kazi wanazozifanya kutumikia nyumba za falme mbalmbali. Kahini haye kapewa jina lake kutokana na matendo yake ya uongo na udanganyifu. Wazee nao pia wamepewa jina kutokana na umri pamoja na matendo yao ya kizee.

**Methali**: ni usemi wa kisanaa wa kimapokeo unaofikiriwa na jamii kuwa kweli na unaotumiwa kufumbia au kupigia mfano na huwa umebeba maana pan kuliko maneno yanayotumiwa. Katika mchezo huu, mwandishi ametumia methali kama vile; hakuna refu lisilo na mwisho….(uk 60), kisichotafutwa hakionekani……(uk 6). Na kadhalika.

**Taharuki:**ni mbinu ya kumwacha msomaji na hamu ya kuendelea kujua namna kitu Fulani au tukio Fulani lilivyoisha. Katika mchezo huu, mwandishi ametuacha na hamu ya kutaka kujua kilichotokea

baada yake Edipode kujitoboa macho, baada ya kifo cha Polibo, baada ya kifo cha Jokasta, yaliyowafika Isamene na Antigone. Na kadhalika.

Na mbinu nyinginezo. Ukisoma mchezo huu utajaribu kuzichambua moja kwa moja ili kukuza Nyanja ya uhakiki.

**N.B**: ***Ikumbukwe kwamba mwongozo huu haubebi yote namna inavyojitokeza katika mchezo, kwa hivyo inakubidi wewe kama mtumiaji kusoma mchezo kwanza na kasha ukasome mwongozo kukusaidia kuelewa vipengele mbalimbali vinavyopatikana na ambavyo vimeangaliwa hapa ndani. Asante!!!***

**TAMTHILIA : KIMYA KIMYA KIMYA**

**MWANDISHI : SAID A. MOHAMED**

**MWAKA: 2011**

**Utangulizi**: tamthilia hii ya kimya kimya iliandikwa na SaidiA Mohamed mwaka wa (2011) ambaye ni mwandishi namtunzi wa tamthilia mwenye kipawa cha aina yake.Mwandishi huyu ametia fora kwa lugha na fasihi ya Kiswahili kupitia maandishi yake. Ana kazi nyingine kama:Riwayayanyusozamwanamke ,RiwayayaDuniayao,Riwaya ya utengano**.**Kwa Tamthilia hii, anaiona jamii ya kesho,leo na kuitabiria yatakayoisibu.

Mvutano baina ya kulia na kushoto umekuwa mzito Mbele hawaendi nyuma hawaendi, kulia na kushoto hawaendi kushoto anataka kwenda kulia, hawezi, kulia anataka kwenda kushoto naye hawezi pia. Kwa kuonyeshana migongo na kuvutana pande zote hawaendi popote. Kushotoanalalama, "mbonasiendimbele? Najitahidi, najivuta, najisukuma lakini……… kumbe sababu yahaya yote ni kimya.

Hali hii itabadilika pale tu watakapokaa kimya, na wakimhusu kimya kusema .mpaka pale, mdogo atamfundisha mkubwa kusema pole pole. Mpaka pale ulimi ulio ganda kwenye baraza la kinywa utakapogunduka. Hapo ndipo kimya kitasema na kitasema kimya kimya kwa sauti kubwa kamaya yoo

**Dhamira Ya Mtunzi**: lengo kuu lake ni kuonyesha athiarimbaya wa kimya yaani; watu kuwa kimya kwa mambo yanayowafikia nakujifanya kama bubu au viziwi .kupitia tamthilia hii, mwandishi yaonyesha dhlima ya umoja katika kupigania haki za binadamu munyonge.

Vile vile, mwandishi amechora mhusikampya kuwa katika mstari wa mbele katika kutaka kujinyakulia amani, nguvu na hasa kazi zao kama wanajamii husika.

Mhusika, mpya anampa sifa za kijasiri na ulimi wake anaupaka maneno yenye asali kuona kwamba kila mwanajamii husika akiyaonja maneno yake apate kufahamu utamu wa kupigania haki zao za kibinadamu

Mpya anawazindua usingizini akina kakaze : Zanga na mussa na hasa wanajamii wenzake kama; Bw.Taja, Bw. Sikilivu na wanajamii kwa ujumla anawafanya waangalie, watoke gizani, wapate kuona wasiwebubu wapate kusema yawahusayo wafukuze kimya kimya kimya kilicholetwa na viongozi kama, Babake Bw. Binafsi, anayedai kuwa amekalia kiti cha enzi.

Isitoshe, mtunzi yataka kuonyesha dhima au nafasi ya mwanamke katika uendelezaji naukombozi wa jamii nyingi duniani. Mhusika kama mpya ni mtoto wake Bw. Binafsi na Bi. Shoo ambaye kila wakati Babake nyumbani na kujuta kwani alimzaa. Mpya kama jina lake anaonyesha mambo mapya yakitendeka mabadiliko tele yakija Bibi huyu mdogo, anaendelea kuwa kichocheo cha wote na mwishowe anafaulu pamoja na wenzake katika harakati za kujikomboa jamii yao. Bi. Shoo, mamake mpya, zanga na Mussa, anamsawisha Bwanake Bw,Binafsi ili awaachilie uhuru watoto wake na wanajamii wanaowavamia kwa nguvu kama za umeme, lakini Bw. Binafsi anakataa, kitambo tu watoto wake wote wanapotoka nyumbani, Bi.shoo naye vile vile anawaunga mkono na wanajamii wengine ili kupigania hai zao kwa ujumla.

Vilevile, mwandishi yataka kuonyesha kuwa viongozi wingi wa jamii husika namna wanavyotaka kukalia viti vya uongozi na kujidai kuwa viongozi wa milele au daima dawamu, lakini mwandishi anatumia taswira yaani, kulia na kushoto kuonyesha mvutano uliopo baina ya watu wanakundi mbili yaani; kushoto yatakaaende kulia nakulia yatakaaendekushoto lakini vyote bure hakuna mafanikio yaani kuna vizingitivinavyo wazunia wote. Mwishowe akina mpya nawanaharakati wenzake wapataujasiri kutokana nakilekisima, na wakadai kuwa nchini tatu tamu zaidi kuliko siasa…….. tokea lini kisima kikasema hiyo ni miujiza lakini kuna siku huenda kikasema! ….wana Imani hiyo na imanina ujasiri huo ukawafanya kufanikishamipango yao na baadaye Bw. Binafsi hushindwa nanguvu zote zakehumwishia.Mwandishi ametumiataswira katika kifunguzi yaani anaonesha kuwa kina wapoteanjia anaonesha kuwa kuna wapoteanjia wawili yaani mmoja anatokea kushoto yamsitu na mwingine anatokea kulia na wote wana hofu ya kupotea, wana shauku kubwa ya kupatanjia sahihi, njaa ya miaka imewabana . kiu ya kame inawaatilisha wanakutana kwenye kisima. Kusima kikavucha maji yasiyotekeka.

Wanapokutana kisimani kulia na kushoto wanalia kiu! Kiu kiu, njaa! Njaa…………. Huko nimetoka kumepoteza maisha vile vile kuna sauti ndani yakisima ambayo hudai kuwa hakuna uhai ahakula maji,. Hakuna ari ya kuskema . Hakuna shime ya kutendanahakuna ushinde na kukshindana na kuchachamaaili kusikkwamaa…………… kwa ujumla mwandishi anataka kuonesha hali ya maisha ilivyo kwa wanajamii husika kwani maisha yao niya nivute ni kuvute.

Kulia na kushoto washangaa sana kusikia sautiile kutokana na kisima wanajisema eti ni kile kisima cha jadi. Ndipo pahala patakatifu walipokutana wahenga kujadili mateso na kutafuta njia ya kuyaondoa………

Waendelea kujiuliza maswali eti “Tokea uni kisima kikasema?

Kwa ujumla mwandishi lengo lake katika kifunguzi hikinikuonyesha vile vizingiti vinavyowazuina wanajamii kuwa na furaha kutokana na uongozi mbaya au mienendo chanya/mibaya ya siasa. Lakini mwishowe kabisa, husema “Ni haki kujifundisha  kusema , hasa ikiwa, hakuna mema” yaani anawatia moyo wale wanyonge wa kihaki ili kujipa moyo wa kusema na kujitoa lara huu unyanyasaji.

Vile vile mwandishi ametumia maonyesho nane kuwasilisha ujumbe wake katika maonyeshohayo, ametumia wahusika mbali wenye majukumu mbali mbali ili kujenga maudhui fulani.

**Uchambuzi wa jalada/ gamba**:

Jalada la tamthilia ya kimya kimya kimya huonyesha picha za watu wawili mmoja akicheka mwengine akimnyamazisha kwa kuweka kidole mdomoni na lengo la kumkatiza kusema. Kulingana na yaliyomo, jalada hili linaweza kuelezwa kwa njia kwamba wanajamii hawakuwa na uwezo wa kusema ndiyo maana ndani kidogo ndipo wanasema kuwa kimya kitakoma wakati mtoto atakapomfundisha mkubwa kusema na pia kuwa ni haki kujifundisha kusema , hasa ikiwa hakuna mema, na kwa hivyo jalada lenyewe huonyesha mambo yalivyo.

**Onyesho la kwanza: (Uk 19 -  24)**

Mazungumzo baina ya kulia na kushoto, kulia na kushoto bado wako kule kisimani na kulia anamuuliza kushoto “unataka kubaki kushoto gani? Y a hali gani? Na kushoto ana mjibu kuwa ya namna mpya, ya uhuru wa kusema, kuandika kulalamika, kutataa na kutoa maoni mwafaka………. Kusho ya manufaa na maaendeleo ya umma ya kujinasibu  kuwa mimi ni mwanachi halisi mwenye laki na nafasi sawa na raia mwingine mimi ninyeliheshimu taifa hili na mimi nitakayehshimiwa na taifa hili hatimaye……Haya yote huonyesha kuwa kushoto na kulia ni wapigania utu, na hata haki zao  binadamu, pengine  twaweza kusema ni wazalendo kulingana namatendoyao papa hapa.

Fauku yahayo, mpya naye anaingia akielekea kwa kile kisima na kuwakuta akinakulia nakushoto wakijivuta wakipeanamigongo ila mmoja wao akitaka kuvuka upande wake na kwenda upande wa mwenzake lakini nyuma au mbele hayendeki kama wanavyodai kwa maneno yao wenyewe.

Mpya anawaambia; Tazameni, tazameni enyi walimwengu, Tazameni wanachi hii Tazameni watoto, wajukuu, vitukuu, virembwe, virembwekeza na vinyinginya…… Tazameni……….. nitazameni mimi mtoto wa Afrika… mimi ninayeshika kiamo kilicho safishwa kwa moshi wa vifuu. Kiamo cha kutekea maji ya ujasiri. Hili ndilo tambiko letu. Tambiko la uhai, Tambiko la kusema ukweli bila ya hofu wala kuogopa ……nakunywa maji ya ujasiri kwa niaba yangu na yenu nikusafisha hofu na woga wangu na natumai woga wenu……. Uk 23

Haya maneno yake yanafanya kamakichocheo cha akina kulia na kushoto  na wananchi nzima kuwatoa uoga nahofu ili kupigania haki zao ili waweze kuwa na nafasi yakutoamawazo yao kifasiri bila kigungumizi chochote. Akisema kuwa wananchi si watawala wanchi yao wajitolea mhanga bure Uk24.

**Onyesho lapili (Uk 25-Uk 44)**

**"Giza totoro na  totoro ya giza**"

Katika onyesho hili-mwandishi anaonyesha kuna giza totoro na totoro  ya giza katika familia ya Bwana Binafsi na Bi.Shoo ambapo Bw. Binafsi nawanafamilia wote wapo wanakula; Binafsi, Bi. Shoo watoto wao akina Mussa, zanga na mtoto wao wa kike yaani mpya ambaye hashangalii ingawa wanafamilia wengine wanamshukuru Bw. Binafsi kwa juhudi zake kwa kufadhili familia yake ingawa nchi nzima hawana chakula chochote na hata chakunywa. Bw. Binafasi anamlaumu mpya mtotowe kwa kumvunjia heshima akisema  ínamisha kichwa na wacha kunitumbulia macho yako makubwa! Wewe kigego, mtoto mkorofi……….sikutaka wewe uingie mimba mwa mamako mtoto wewe. Mtoto wa kike ana faida gani? Uk 34. Vile vile, hunyesha kuwa Bw. Binafsi ni mbaguzi kwani anabagua watotowe kulingana najinsia zao…………….

katika nayesho hili kuna sauti  Fulani ikijitokeza ikisema "A-a, Bi. Mpya, hapa kwenu watu hawasemi waziwazi wala hawasemi kwa kelele, Hawamruhusiwi  kufanya hivyo! Uk 27. Sauti inaendelea  "Hatari au labda ajali, shauri upepo umeanza kuruma. Aaa-labda ajali mara moja ni la kioja. La kipekee tuko hili. Hapa petu hapajaanza……….. ni wakati mapya anaposema kuwa yeye tayari ameanza kuzungumza waziwazi Uk 28.

Pengine, mpishi anasema kuwa upepo umekuwa mwingi sana na hata vyombo vinaanguka jikoni akisema "nyinyi vyombo mmetumwa nini kuja kunisemesha mimi? Kuja kunimwagia unga. Mimi sijapata kusema namna hii………mnasema nyinyi na kunisemesha mimi kwa nini? Ni wakati mpishi huyu anapotengeneza chai kwa wanafamilia hiyo wakiwa wote Wagonjea chai lakini upepo huo niishara ya mabadiliko makubwa. (Uk 29)

Baada ya Bw. Binafsi kumfokea mtoto wake mpya mkali kwa kumdharau na kumwona kama jitu bure ambalo halina manufaa kwake, mpya akaamua kwenda zake akisema akisema kwa sauti yake "Huyu ndiye baba'angu …….mtu wa ajabu! Nafsi yake niyake mwenyewe. Lakini nafsi zetu si zetu nafsi zetu ni ……….aa sisemi- simhusiwi kusema………(Uk 30-31) nimechoka kusubiri; nimechoka kungojea, kunyamaza huku kunyamaza najua ndiko kunakomani gamiza mimi na wote nchini humu………Uk 31

Akina Musa na zanga wanamsifu baba yao Bw.Binafsa kwa vile ambavyo amewa-fanyia kuidumisha familia yao, lakini kwa upande mwingine Bi.shoo na Binti yake- mpya kukazuka utengano na mzozo mkali kwao na Bw. Binafsi kwani anawalaani akisema “mtalaaniwa nyinyi, mtakosa radhi zangu, mtakosa kila kitu………Uk 42)

Bw.Binafsi anaghadhibika baada ya mpishi kumwelezea kuwa upepo umeendelea kuvuma na kuangusha vyombo kokote na kusema eti wacha vyuma vianguke na kelelezienee nyuma na mbele! Waache waende wanaotaka kwenda nasema wacha waende! Najua watarudi hapa hapa wale……….. najua wataja hapa kuombaradhi……….kimya …kimya………….kimya……..Uk 43.

**Onyesho la tatu (Uk 45-56)**

“**Mdogo humfundisha mkubwa kusema”**

Baada ya siku kadhalika Bi. Shoo na watoto wa kiume wanarudi nyumbani kama vile Bw. Binafsi alivyotabiri kuwa watamrudia……

Zanga na Mussa wako nyumbani zanga yumo kitandani mwake na halafu anasikia sauti ya dada yake mpya ikimnongenezea masikioni (Uk 49) sauti hiyo inawasawisha ndugu hao na kupiga mioyo konde ili waweze kujiunga nadada yao-mpya ili waweze kujikomboa kihaki ili mdogo aweze kumfundisha mkubwa kusema.

Sauti ya mpya ikiwasawisha ndugu zake eti, ndani na nje ya majumbani mwetu ni sawa sawa. Hakuna tofauti , wanaotawala ndani na nje ni baba zetu. Nje kunakandamizwa kama tunavyokandamizwa ndani. Tatizo ni kwamba Sisi waafrika tunadhani utawala wandani na nje ya nyumba ni utawala wa uzazi. Mtawala mkuu ni baba yetu na mkewe ni mama yetu. Kwa maoni yangu utawala wa ndani kiasi Fulani lazima uchangie taifa nzima …………..usiwe utawala wa mtu mmoja na familia yake finyu ingawa pana………..Uk 53.

Sasa, zanga na Mussa wanaanza kujiuliza maswali? Je! Tutawafunzaje watu wengine kusema tukiwa sisi hatujui vizuri kusema? Lakini sauti ya mpya yawatia moyo kuwa wataweza Uk 54

**Onyesholanne (Uk 57 – Uk 62)**

**Kero na wanaokereka…..**

Ndani kumezaa nje,

Na nje kumezaa mchakato wa umma.

Bustani ya taifa jijini, wananchi wanaanza kukusanyika kwa mkutano wa dharura. Wanaingia mmoja mmoja wawili wawili nahatavikundi vikundi ………………Uk 57, Bw. Taja, Bw. Sikilivu, Bi. Subira, Bi.Ugeni wote waja na kuanza kulalamika juu ya masula yanayowakera kama wanajamii, kwamfano Bi.Subira husema "*mchakato ndio huu uliotuleta hapa Huwezi kujikomboa kama husemi, miti inakatwa ovyo, watu wanajenga makazi au nyumba bila ya vibali, ardhi au viwarija vya watu hudukuliwa hivyo hivyo***……….. *Uk 59.***Wanareli waanza kuimba nyimbo za ukombozi na kupiga kelele. (Uk 60-62)

**Onyesho la tano: (Uk 63 – 90)**

**Wasi wasi wa wazee**

Bw. Binafsi-ambaye ni kiongozi wa Taifa hilo lao anawaita akina waziri wananchi na ofisa wausalama wanaingia ofisini mwake na kuripoti vile ambavyo vinaendelea nchini nzima………..Uk 63,

Bw. Naona anamwelezea kuwa mambo hatari yaja kulinganana vile aonavyo watu wenye shauku kubwa yakutaka haki zao kibinafsi.

Akisema kuwa inasemekana, watu wana….. watu wanasema kwamba mambo yalianzia nyumba kubwa mheshimiwa kiongozi mkuu. Watoto watatu wa nyumba kuu, Mussa, zangu na mpya ndio waasisi wa fikra hizi mpya na hata mbaya. (Uk 67)

Bw. Binafsi anawaamuru kuwakamata watoto hao wote bila kujali ni watoto wa nani?

Bw. Salamina na Naona wapewa jukumu kubwa la kusimamisha wananchi ili wasiendelee kusema bila kujua wameishajua umuhimu wa kusema nakutupilia mbali kimya kimya kimya kilichowafumba macho zama za kale na sasa husema tumechoka, haya yote yatosha………….

**Onyesho la sita**

**(Uk 72 – Uk 75)**

Wakati ukifika watu husema wakatiumewadia .

Sasa sauti ya mpya yakutanana ile sauti ya umma na kuitikia nakusema kuwa mpya yote asemayo ni ukweli kwao kwa kusema "Tumekubali…………… tumekubaliyote. Tukopamojanawewetukotayari- Tuko tayari kuingia njiani kwa nidhamu nzima , Bila ya uchokozi, bila ya fujo……Uk 73

Sauti ya mpya inasikika ikiwelezea muhimu katika yote kama. Kuandaa katibavilivyo kusimama kidete tudai kugeuza mwenendo wetu wa kutofali makslahi yetu yakitaifa kuhakikisha kuwa wananchiwapata huduma za kijamii nchini mwetu, tupigane vita kwa ushujaa kuondoa ufisadi na kulinda nchi yetu na pia tuzilinde rasilimali zetu zisiiibwe kiho-lela, twataka ndii iwe yetu sote………..Uk 73-74

**Onyesho la saba : (Uk 77 – Uk 82)**

**Baba anataka kuwala watoto wake**

Bw. Binafsi anaingiwa na wasiwasi, mwingi kusikia eti keleleza wanajamii zaendelea kuvuma…. Uk 77 vile vile kuna wimbo unaoimbwa "Haki ni kamaupanda …

'**usipoitekelezautajutia—**

**'leo na kesho ndiyo**

**'kesho na keshokutwa sawa**

Bw. Binafsiyawageukia – kimya kimya kimya mnaimbanini nyinyi? Mnanifanyia inda siyo?........Uk 77

Bw. Binafsi hana nyuma wala mbele kicheko cha kijeli chaendelea mpaka anapoenda kumuuliza sauti ya yoo naye akasema "Nilikwambia zamani mwenendo wako ukanidharau……….. nilikwambia wewe binadamukama itakavyo kuwa ……………… wewe si mungu wala malaika………… kisha nikakwambia ukitawala kwa wema utamalizia wema……………. Uk 82.

**Onyesho lanaane: (Uk 84 – Uk89)**

**(si shwari tena)**

Sauti za wananchi zajumuika na Bi.Shoo anasawisha Bw. Binafsi aepuke na uongozi yaani watu wamemchoka lakini anakataa….. Uk 84

Bi.shoo anamwelezea **Bw. Binafsikuwaleoameambiwakuwasualalanchiameligeuzalakifamilia**!....... si tokea kale na kale suala la ndi hii limekuwa sualala kifamilia? ……..**namambo ya nyumba kunga, na kuta za kuungaunga**? Mbona **usemihuu**leo?

Mwishowe kabisa Uk 89, kulia na kushoto kwa kifungio, wanaimba pamoja,

**mwisho maana yake mwisho**

**Mwisho hauwezi kuwa mwanzo**

**Mwisho unapokuwa mwisho**

**…………………………………………. (Uk 89.**

**<u>MAUDHUI YALIYOMO</u>**

**Siasa** : Maudhui ya kisiasa yanajitokeza sana katika tamthilia hii kwani ndilo lengokuu hasa, kwamfano mwandishi ameonesha utawala mbaya wa viongozi wingi wajamii za kiafrika akitumia mfano wa Bw. Binafsi anayechukua mambo ya umma kama familia yake kwamfano Uk 85, Bi.shoo anaposema "leo hii ndio naambiwa kwamba juala la nchi nimeligeuza la kifamilia?.......................... na mambo ya nyumba kuta za kuungaunga? Mbona usemi huu leo..?...

Vile vile sauti yaYoo inapomwelezea Bw. Binafsi baada ya mambo kumwendea mramana kusema "nilikwambia zamani mwendo wako ukanidharau- nilikwambia eti wewe ni binadamu tu …… wewe si mungu wala malaika …. Uk 82

**Ndoa**. Suala la ndoa hujikita katika tamthilia hii ambapo kuna Bw. Binafsina mkewe B.shoo, wana watoto watatu yaani mmoja wa kike- mpya na wawili wa kiume – mussa na zanga. Bw. Binafsi kama mkuu wa familia anajaribu kufadhili familia yake ingawa anapata upinzani kutokana na baadhi ya wanafamilia wake.

**Mapenzi:** vile vile jambo la mapenzi hukidhihirisha sana katika Tamthilia yaani, mwanzoni familia ya Bw. Binafsi, Bi.shoo na hata **watoto**wao, mpya Mussa

Nazanga, wanapendana ingawa baadaye wanapata utofauti kwa mafikirio au mitazamo mipya kwa mienendo yakisiasqa.

**Nafasiyamwanamke**: mwandishi amechora mwanamke kwa pande mbili yaani mwanamke kwa jamii husika huangaliwa kama kiumbe duni kulingana na maneno ya Bw. Binafsi akinukiwa akisema *:**sikutakaweweuongeemanenohayomakali***kwabintiyempyaambayeanatakakuletafikirazake mpya nahataza kigeni **isitoshe**, mwandishi ameonesha mwanamke kuwa mzalendo, jasiri na wenye juhudi kulingana na matendo ya mpya na mamake Bi.shoo katika ukombozi wa nchi yao ambapo Bi.shoo anaamua kufuatia watoto wake……………..Uk 43

**Mabadiliko:** Tamthilia yenyewe inazungumzia juu ya mababadiliko ambapo mwandishi husema "***mdogo humfundisha mkubwa kusema***" hayo ni mabadiliko wanayopigania yaani wanajamii wamechoka na kimya kimya kwa kila jambo, kulingana na maneno yake Bi. Subira Uk 59 akiwa analalamika, kuwa watu

huchafua mazingira, ofisi zetu chafu, hatanafsi zetu ni chafu…. Ba kwa hiyo, mabadiliko ni suala muhimu sana.

Fauku ya hayo**,** mabadiliko hujitokeza wakati upepo unapovuma nyumbani mwa Bw. Binafsi na kuvunja vikombe na vifaa vinginevyo na mwishowe wanafamilia yake kutoweka, wananchi kujikusanya kwa afisi yake akina Bw.Sikilivu, Taja Bw. Subira nk Uk 57.

**Itikadi ya miungu**, Mwandishi amefaulu sana kwa kutuonyesha imani na itikadi na miungukatika tamthilia hii kwa kutumia mbinu ya taswira ambapo kisima cha jadi hutoa sauti Fulani yenye ujumbe waukombozi. Kwa kisima hiki, ndipo mpya anakutana na kushoto nakulia wakapiana migongo, ………..

nampya anapata maji ambayo anadai kuwa ni maji yenye kuwatoa uoga na kuwa na ujasiri.

**Isitoshe mwandishi ameonesha maudhui ya umoja** namuhimu wake, wakati ambapo wanchi wakajumuika kwa ofisi ya Bw.Binafsi wakidai haki zao, kwamfano, Bw. Sikilivu, Bw. Taja na Bw. Subira Uk 57 – 59 na mwishowe wanafaulu na hoja yao.

**Migogoro/mizozo**: Hujitokeza kati ya mpya na babake Bw. Binafsi baba akidai kuwayeye hamheshimu hata kidogo.

Vilevile, Bi.shoo, watotowe akinazangua Mussa na mpya kujiunga pamoja dhidi ya Bw. Binafsi ambaye hataki kuepuka kile kiti asemacho kwa ni cdhia enzi daima dawamu.

Pengine, migogoro kati yawananchi na viongozi waserikali yao ambao hudaiwa kuwa hawajali.

## <u>HULKA/ TAWASIFU/TABIA ZA WAHUSIKA</u>.

Mtunzi amechora wahusika wake katika mchezo huu kulingana na lengo lake, yaani wahusika wengi huegemea sana kwa suala la ukombozi wan chi yao ambayo imekaa kimya na kimya kikatawala.

**Mpya**: ni mtotot wa kike wa bwana binafsi na bi shoo. Kama jina lake, ni mwenye matendo mapya ambayo anajaribu kuleta nchini mwao.

- Ni mzalendo ambaye anapenda na kupigania nchi yake ingawa babake anamtisha sana.
- Ni jasiri kwani ujasiri wake unadhihilika wazi wakati anapotoka nyumbani na kuchochea wengine jamii nzima waweze kuamka na kupigania haki na uhuru wao.
- Ana Imani kwa mila na desturi za kwao ndiyo sababu anakwenda mara kwa mara kwa kisima ambapo anakutana na kulia na hata kushoto wakavutana na

- kushangaa sana wanaposikia kuwa kisima kinasema. Wote wanaamini kuwa hicho ni kisima cha mababu zao ambapo wangekusanyia na kuzungumza masuala yawahusuyo.
- Ni mwenye hasira ndiyo sababu babake wakati wanapokula akimwangalia kuwa mpya hafurahii chakula na kuanza kumtusi, kwa hasira mpya anatokomea moja kwa moja.
- Ni mshawishi kwani anawashawishi kaka zake; mussa na zang, mamake na hata wanajamii kumuunga mkono katika harakati za ukombozi.

**Bwana Binafsi**: ni bwanake Bi shoo, baba yao mussa, zanga na mpya.

- Ni kiongozi mbaya kulingana na malalamiko ya wanajamii kama vile; bwana Taja, sikilivu na Bi subira ambao wanalalamika juu ya uongozi wake mbaaya.
- Ni mwenye hasira kwa kuwa anakasirika wakati mpya anakataa kula na anaendelea kumtusi kwa kusema mtoto wa kike hana faida yoyote
- Ni mpenda cheo/ heshima au uongozi kwani bibi yake anamshauri ili aweze kuwachia watu uhuru a haki zao lakini anakataa mpaka mwisho anapopata msiba mkali.
- Ni mkatilli kwani yeye hasikilizani vyema na watawaliwa wake na hasa hasa wanafamilia yake.
- Yeye ni mbaguzi. Kulingana na maneno yake anaonyesha ubaguzi wa kijinsia anaposema 'mtoto wa kike ana faida gani?'

**Bi shoo**: ni mkewe bwana binafsi na mama yao; mussa, zanga na mpya.

- Ni mpenda umoja na usawa ndiyo maana anamshauri bwana yake kuwachilia wanajamii na hasa watoto wake uhuru na haki zao ingawa yeye anakataa.

- Ni mwanaharakkati kwani naye vile, anjiunga na watoto we na wanajamii kwa ujumla kupigania haki na uhuru wao.
- Ni mwenye huruma kwa kuwa anamhurumia mtoto wake mpya anapotoka nyumbani baada ya babake kumtusi.
- Ni mzalendo kwa kuwa anapenda nchi yake ndiyo sababu anaipigania ili watu waweze kuamka usingizini na wajitawale badala ya kuachilia kimya kutawala daima dawamu.\

**Mussa na zanga**: ni kaka zake mpya na watoto wao bwana binafsi na bi shoo.

- Ni wazalendo kwani wanajiunga na wanajamii husika ili waweze kujinyakulia Amani, uhuru na haki zao.
- Ni jasiri kwa kuwa ingawa baba yao ni mkali kama samba na mwenye vitisho viingi, wanasimama imara na kupigania haki zao wenyewe na wanajamii wenzao.
- Ni washilikiani yaani ni wenye umoja ndiyo sababu wanajiunga na dada yao mpya na baadaye wanajamii wote.

**Bwana Sikilivu, Bwana Taja Na Bi Subira**: ni wanajamii ambao wanaitika mwito wa mpya ili kupigania haki na uhuru wao.

- Ni wazalendo.
- Ni jasiri.
- Ni washirikiani maana yake wana umoja.
- Ni wana mapinduzi.

**Bwana Naona:**ni waziri  wa nchi ambayo bwana binafsi anaongoza.

- Anatimiza malengo yake ndiyo maana anaripoti kwa bwana binafsi mawazo ya wanajamii ingawa binafsi anamraumu kwa utomshauhri na kuacha mambo yaka hivyo hivyo.

**Bwana salamina**: ni afisa wa usalama katika serikali inayoongozwa na bwana binafsi. Katika uungozi wake ndimo migomo ya haki za watu yanajitokeza. Naye vile vile bwana binafsi anamraumu kwa kutotimiza lengo lake.

**<u>MBINU ZA UANDISHI:</u>**

Ni vipengele mwandishi anavyotumia kuwasilisha ujumbe wake.

1. **Taswira**: mbinu hii humaanisha ujenzi wa mawazo na picha akilini mwa msomaji. Kwa mfano kushoto na kulia kuvutana kando ya kisima na hata kusikia kisima kikisema, hujenga picha Fulani akilini mwa msomaji. Na pengine mdogo kumfundisha mzima kusema nayo vile vile ni taswira.
2. **Majazi**: kumpa jina mhusika kulingana na sifa zake au matendo yake. Kwa mfano jina mpya limetumiwa kuonyesha upya wa mambo ambayo yeye mwenyewe anayaleta. Isitoshe, bwana binafsi amepewa jina hilo kwani anajipendelea na haajali wengine ndiyo sababu anasema ‘wengine hawana chakula lakini nyinyi chakula nyumbani cha tosheka…..’ akiweelezea wanafamilia yake.

3. **Takriri:** hii ni mbinu ya kurudia rudia neno au fungu la maneno ili kuonyesha msisitizo wa jambo Fulani. Kwa mfano kichwa chenyewe, 'kimya kimya' huonyesha namna kimya kinavyotawala jamii nzima.
4. **Malumbano/ majibizano/ mazungumzo**: hii inahusu wahusika mbalimbali kuzungumza kwa zamu. kwa mfano katika kitangulizi kulia na kushoto wanajibizana wanapokutania kando kando ya kisima na kuulizana maswali kama kisima chaweza kikasema? .

Na mbinu nyinginezo: ukiendelea na kuisoma tamthilia yenyewe unaweza kuichambua na kuelewa mengi yanayoihusu.

**N.B**: ***Ikumbukwe kwamba mwongozo huu haubebi yote namna inavyojitokeza katika mchezo, kwa hivyo inakubidi wewe kama mtumiaji kusoma mchezo kwanza na kasha ukasome mwongozo kukusaidia kuelewa vipengele mbalimbali vinavyopatikana na ambavyo vimeangaliwa hapa ndani. Asante!!!***

**MCHEZO: CHEMA CHAJIUZA**

**MWANDISHI: INNOCENT AGUME**

**MWAKA: 2018**

**Muundo Wa Tamthilia.**

Muundo huwa ni mtiririko wa visa na matukio katika kazi za kifasihi. Hapa, tutaangalia jinsi mwandishi Innocent alivyofuma matukio kwa muhtasari kutoka kitendo cha kwanza hadi kitendo cha nne na mawazo makuu yaliyomo.

**Kitendo Cha Kwanza.**

**Onyesho La Kwanza.**

Hapa, tunamuona Bwana Kwatampola nyumbani kwake kakoba anazungumza na mke wake Kunihira juu ya kukosa kumkuta Mzee Bumaali.

Bwana Kwatampola tunamuona baada ya kuambulia patupu anapanga miadi na mtumishi kumpigia simu ili amkute Kabaila Bumaali.

Pia, tunamuona Injinia Bakehena anafutwa kazini na analalamika juu ya kabaila bumaali kwa kumfukuza.

Vilevile, tunamuona Kunihira analalamika juu ya mume wake kwamba labda alirogwa kwakuwa pesa anazozipata kutoka kwa Bumaali hazitumiki vyema iwezekanavyo.

**Onyesho La Pili.**

Hapa tunamuona Bumaali na Kwatampola wameketi uani. Bumaali anamwelezea Kwatampola kwamba alipata kidosho na anataka akitengenezee jumba huko Nyamitanga. Bumaali amempa Kwatampola milioni thelathini (30) ili ashughulikie kazi nzima ya kujenga ugo halafu atajenga jumba zima. Milioni thelathini ni za vifaa na vibarua. Bumaali anamwambia Kwatampola kwamba injinia bakehena alimuibia pesa na asimsaliti kama yeye.

**Onyesho La Tatu.**

Hapa, tunawaona Mzee Bahemuka na mke wake Bi-Shogora njiani wanamtembelea mwanao Kwatampola huko kwake Kakoba. Mzee Bahemuka anatembea kwa kuinama na na kuiweka

mikono yake juu ya mkongoji alioulaza mabegani kwake. Bi-shogora na mumewe Bahemuka wanatembea wakizungumuzia juu ya mtoto wao kwamba ni maskini mzuri tena mwadilifu. Tunawaona wamefika Kakoba nyumbani kwa Kwatanpola mtoto wao, mke wake Kwatampola Kunihira anawakaribisha kwa heshima na kumpa mcheja wake Bi-Shogora maji ya Rwizi ya kunywa kupuuza joto la njia. Papo hapo, Kunihira anawaelezea kwamba mtoto wao babake Ben yumo kitandani na Ben mwenyewe ameenda shuleni.

Vilevile, Kwatampola anakuja kutoka kitandani na kuwasalamia badaaye anaondoka nje na babake halafu Kunihira akabaki nyumbani na mcheja wake Bi-shogora wakijadiliana.

Baada ya muda mchache, tunawaona Bahemuka na mke wake bi shogora wanaondoka kurudi kwao Rwampala.

**Kitendo Cha Pili.**

**Onyesho La Kwanza**.

Hapa, tunawaona Kwatampola na mkewe Kunihira nyumbani kwao wanazungumuza pamoja. Kwatampola anamwambia mkewe kwamba Mzee Bumaali amemuita asubuhi na kumpa kandarasi ya mradi kujenga ugo na badaaye atajenga jumba zima huko Nyamitanga.

Tunawaona pia Kwata na mkewe Kuni wanaondoka kwenda kule Nyamitanga pale jumba litakapojengwa. Tunaona Kuni amepewa kazi ya kupikia wajenzi wote na kwata anawasimamia wajenzi wake.

**Onyesho La Pili**.

Hapa, tunamuona kabaila Bumaali anamshukuru kwatampola kwa kujenga ugo vizuri na kwa muda uliokuwa unatakikana. Bumaali anampa kwata bunda la noti ya shilingi milioni mbili ili azigawanyie vibarua wake kwa kazi waliyoifanya na Kwata anashukuru sana.

Pia, tunamuona Bakehena anazungumuza na Kwatampola kuhusu masuala ya pesa alizopewa na kabaila Bumaali halafu anaenda maramoja hadi nyumbani kwa kwata na kumwelezea Kunihira kwamba mume wake Kwata amepewa hela nyingi sana na ameenda mjini mbarara kuzitumia ovyoovyo.

Tunamuona Kunihira baada ya kusikia ujumbe huo anashutuka na kumuita Ben kwa kumtusi kwamba ni mjinga kama babake kwa hasira. Papohapo, tunamuona Kwata anaingia. Mkewake anaanza kulalamika juu ya ujumbe alioupokea ya kwamba amepewa hela na ameenda mjini kuziharibu kumbe kwata alikuwa ameenda kuvinunua vifaa vya ujenzi.

Tunamuona Kunihira maramoja anaingia nyumbani na kuchukua begi yake kubwa na kurudi kwao Kabale. (talaka inafanywa). Tunamuona Ben mtoto wao analia juu ya kuachwa na mamake lakini babake Kwata anambembeleza na halafu anamtwaa Rwampala kwa mzee Bahemuka na Bi-shogora ili wamlee hadi mamake atakaporudia.

**Onyesho La Tatu**.

Hapa, tunamuona Kwatampola na wajenzi wake mkutanoni huko Nyamitanga katika uwanja wa ujenzi. Kwata anawagawanyia hela alizopewa na kabaila Bumaali juu ya kazi nzuri waliyoifanya ya kujenga ugo.

Tena, Kwata anawaelezea wajenzi kwamba alikumbwa na vita vya kibinafsi, tamaa na mwishowe mke wake akamuacha.

Wajenzi wanakabidhiwa hela na kila mtu akachukuwa shilingi **36956**.**52**. Wote wajenzi wanamshukuru kwata na kabaila Bumaali.

**Kitendo Cha Tatu.**

**Onyesho La Kwanza**.

Hapa, tunamuona Kunihira Nyamitanga katika uwanja wa ujenzi tena jikoni kwa upishi anawahudumia wajenzi.

Tunawaona wajenzi wote na mainjinia wanafanya kazi kwa bidii.

**Onyesho La Pili**.

Hapa, tunawaona kwata na mainjinia watatu wanaongea kwa sauti za chini sana.

Injinia wa tatu anamwambia kwata kwamba yeye ni msomi hataki vitu vya upesiupesi. Pia tunamuona injinia huyo anamshukuru kwata kwa kazi nzuri.

**Onyesho La Tatu**.

Hapa, tunamuona Injinia Bakehena nyumbani kwake chumbani mwake anazungumuza na mke wake Nabaganzi. Nabaganzi anamwambia mume wake kwamba kabaila Bumaali anamtangaza kwa marafiki zake wote ya kwamba alimuibia pesa.

Pia, tunamuona Bakehena anapanga kuelekea mjini Fortportal kutafuta kazi ya kufanya ili naye aajiriwe kama wengine.

**Kitendo Cha Nne.**

**Onyesho La Kwanza**.

Hapa, tunamuona Nabaganzi anaongea na kwatampola katika uwanja wa ujenzi huko nyamitanga. Tunaona kwatampola amempa Nabaganzi kazi ya ufagizi na anashukuru sana.

**Onyesho La Pili**.

Katika onyesho hili, tunawaona Bumaali, Akello na wajenzi wote huko Nyamitanga katika kasri na wanakagua kazi waliyoifanya kwa muda.

Kabaila bumaali anashukuru sana Kwata hadi kiasi cha kumbusu mkononi juu ya kazi nzuri aliyoifanya na wajenzi wake wote.

Pia, tunamuona injinia wa pili anahakikisha uzuri wa Bwana Kwatampola kwa kusema kwamba hata mitaimbwa, rangi na mabati viliibwa lakini Kwata alitumia pesa zake mwenyewe kununua vipya.

**Onyesho La Tatu**.

Hapa, tunaona wageni washerehekeaji wakiendelea kumwajika wakiwemo wafanya biashara mashuhuri, wanasiasa, wanadini wake na waume wote Nyamitanga uani wa kasri la Machu.

Pia, tunawaona wageni waalikwa na wasioaalikwawote wanakaribishwa. Mziki unaendelea kupigwa polepole na Mc-bob king. Watu wote wamefurahi sana.

Bwana harusi Bumaali na Bi-harusi Machu nao wanakaribishwa. Mziki unadundwa tena na Mc.Bob king mfawidhi.

Vilevile, tunaona Bumaali anatoa hotuba kwa kushukuru kila mtu na mke wake wa kwanza Bi-Akello.

Bumaali anazawadia kwatampola juu ya wema wake kwa kumpa kisanduku chenye funguo na hati ya maandishi yaliyo ya kumpa jumba hilohilo alilojengea Machu la Nyamitanga.

Bila shaka tunamuona Kunihira anatoka shoti juu ya yale aliyoyasikia na wanakuja kumhudumia kwa kumuzoea pale alipokuwa ameanguka. Kunihira anapelekwa Mbarara Regional Referal hospital. Bumaali anahitimisha kwamba atarudi kwake Makenke na wake wake wote wawili na kumwachia kwata jumba la Nyamitanga.

## WAHUSIKA NA SIFA ZAO

**Wahusika**ni viumbe hai au visivyohai vinavyoshirikishwa katika kazi yeyote ya kifasihi ili kujenga maudhui na dhamira ya mwandishi.

Hivyo basi, katika tamthilia hii ya chema chajiuza, kuna wahusika kadhaa mwandishi aliowatumia kufikisha ujumbe wake kwa hadhira na baadhi yao ni;

**Kwatampola**: Mhusika huyu ana sifa zifuatazo;

- Ni mhusika mkuu kwani tunamuona anajitokeza aghalabu katika tamthilia nzima.
- Ni mzazi kwani tunamuona katika tamthilia anambembeleza mtoto wake aitwaye Ben. (uk 23)
- Ni mume kwani katika tamthilia tunamuonandiye aliyeoa Kunihira.
- Ni mwanake Mzee Bahemuka na Bi-Shogora kwani tunawaona wanakiweza wakati walipomtembelea kwake Kakoba.(uk 23)

- Ni mfanya kazi kwani tunamuona hata alizawadiwa juu ya wema wake katika kazi ya kujenga jumba la Machu huko Nyamitanga.(uk 115)
- Ni mtiifu kwani tunamuona katika tamthilia anamtii mwajiri wake Kabaila Bumaali hata kufika kiwango cha kutomuita jina lake bali kumuita Mzee.
- Ni mwenye mapenzi kwasababu kinawekwa wazi katika tamthilia na mke wake Kunihira wakati alipo toka shoti akaacha karamu akaenda naye hostitalini. Pia anampenda mtot wake Ben kwa kumuimbia nyimbo za kumbembeleza baada ya mamake kufanya talaka(uk 47)

**Kunihira**: Mhusika huyu ana sifa zifuatazo kulingana na jinsi anavyochorwa katika tamthilia.

- Ni mke wake kwatampola kwani hata tunaona katika tamthilia anamuita Bi-Shogora mcheja wake tena ndiye anayechorwa kama mke wake kwata katika mchezo. (uk 49)
- Ni mhusika mkuu kwani tunamuona anajitokeza aghalabu katika vitendo vyote.
- Ni mamake Ben kwani tunamuona katika tamthilia anamuacha mtoto Ben na kufanya talaka. (uk 25)
- Ni mjasiri kwani tunamuona katika tamthilia anajiunga mkono na wafanya kazi wa kiume na kuwapikia au kuwahudumia kama mpishi. (uk 32)
- Ni mvumilivu kwani tunamuona anavumilia maisha yao ya kimaskini na mume wake Kwata hadi walipobadilika kuwa watajiri.(uk 27)
- Ni mtiifu kwani anamtii mume wake Kwatampola kwa kuitika wito wa kupikia na kuishi na vibarua.
- Ni mwenye mapenzi kwani kinawekwa wazi katika tamthilia ya kwamba alivumilia umaskini wao pamoja mumewake Kwatampola, hakuna mapenzi yanayozidi uvumilivu huo. (uk 27)
- Ni mfanya kazi kwani tunamuona anahudumia vibarua kwa kuwafanyia kazi ya kuwapikia huko Nyamitanga. (uk 32)

**Bumaali**: Mhusika huyu ana sifa zifuatazo kulingana na jinsi anavyochorwa katika tamthilia ya chema chajiuza;

- Ni mume kwani alimuoa Bi-Akello na Bi-Machu hasa katika sherehe za kumuoa mke wa pili (uk 113)
- Ni kabaila au mtajiri mkubwa sana kwani ana nyumba nyingi mjini Mbarara na tena alipompa Kwata milioni 30 ni ishara ya utajiri. (uk 13)
- Ni mume wao Bi-Machu na Bi-Akello kwani anawatambua wakati wa sherehe za kumuoa Machu mke wake wa pili huko Nyamitanga. (uk 113)
- Ni mwenye mapenzi kwani tunaona katika tamthilia anamjengea jumba Machu na anakiweka wazi pale ambapo tumemuona anamsimulia Kwata kuhusu kidosho chake alichopata huko Rwebikona, huo ni upendo wa kiwango kikubwa kubwa. (uk 116)

**Bi-Akello**: Mhusika huyu ana sifa zifuatazo kulingana na jinsi anavyochorwa katika tamthilia ya chema chajiuza;

- Ni mkewe wa kwanza wa Bwana Bumaali kwani kinaoneshwa katika tamthilia katika sherehe za kumuoa mke wa pili Bi-Machu. (uk 113)
- Ni mvumilivu kwa kuvumilia maisha ya kuolewa kwa mke wa pili kwani si rahisi hata hakipatikani mtu kuvumilia kama yeye hasa katika kizazi cha leo.(uk 112)
- Ni mtiifu kwani anamtii mume wake Bumaali kwa kukubali yote aliyomwambia.
- Ni mwenye moyo wa kupa kwani tunamuona anakubali kumpa zawadi kwatampola kwa kazi aliyoifanya.(uk 105)

**Bi-Machu**: Mhusika huyu ana sifa zifuatazo kulingana na jinsi anavyochorwa katika tamthilia ya chema chajiuza;

- Ni mtoto wa Daudi kwani tunawaona Kwata na mke wake wanasema kwamba, kunihira atakuwa mcheja kwake kwani wana uhusiano yao na Daudi.(uk 29.)
- Ni mwenye mapenzi kwani alikubali harusi juu ya mapenzi.(uk 113, 116)

**Nabaganzi**: Mhusika huyu ana sifa zifuatazo kulingana na jinsi anavyochorwa katika tamthilia ya chema chajiuza;

- Ni mke wake Injinia Bakehena kwani tunawaona kwao baada ya kufutwa kazini wanazungumuzia jinsi ya kutafuta kazi (uk 81)
- Ni mjasiri kwani anajiunga na wajenzi huko Nyamitanga kwenye uwanja wa wajenzi na kufanya kazi ya ufagizi bila kuogopa. (uk 90)
- Ni mwenye mapenzi kwani tunamuona anakubali kuishi na mume wake Bakehena hata baada ya kufutwa kazini.(uk 81)
- Ni mvumilivu kwasababu ukweli unaonekana pale alipoamua kufanya kazi ya ufagizi huko kwenye uwanja wa ujenzi Nyamitanga. (uk 90)
- Ni mfanya kazi kwani tunamuona anaacha familia yake na kwenda huko Nyamitanga kwenye uwanja wa ujenzi na kufanya kazi ya ufagizi bila kuaibika kama mwanamke aliyekuwa mtajiri muda mchache nyuma. (uk 90)

**Bahemuka**:Mhusika huyu ana sifa zifuatazo kulingana na jinsi anavyochorwa tamthiliani chema chajiuza;

- Ni mume kwani ni mume wake Bi-Shogora kwani tunawaona wote wanakaribishwa nyumbani kwa kwatampola. (uk 23)
- Ni babake kwatampola kwani tunamuona Bahemuka alipokuwa anaelekea kakoba anazungumuza na mke wake kwamba walimzaa mtoto maskini mwadilifu na mwema na atazikwa na wengi. (uk 21)
- Ni mwenye mapenzi. Je kwatampola alitoka wapi? Ni juu ya mapenzi kati ya Bahemuka na Bi-Shogora. Pia, anampenda mtoto wake Kwata ndipo akamtembelea (uk 23)

**Bi-Shogora**: Mhusika huyu ana ssifa zifuatazo kulingana na jinsi anavyochorwa katika tamthilia ya chema chajiuza;

- Ni mke wake mzee Bahemuka.
- Ni mzazi kwani ndiye mamake Kwatampola kulingana na tamthilia.(uk 23)

- Ni mwenye mapenzi kwani isipokuwa mapenzi asingemtembelea mtoto wake Kwatampola kumuona huko Kakoba, huo ni upendo wa mama kwa mtoto. (uk 23)
- Ni mtiifu kwani anamtii na kumheshimu mume wake Bahemuka.

**Bakehena**: Mhusika huyu ana sifa zifuatazo kulingana na jinsi alivyochorwa katika tamthilia ya chema chajiuza;

- Ni mwizi kwani tunamuona katika tamthilia aliiba pesa za kabaila Bumaali mwajiri wake na kufutwa kazini. (uk 13)
- Ni mwenye mapenzi kwani anampenda mke wake Nabaganzi. (uk 81)
- Ni mfanya kazi kwani tunamuona ni injinia mjenzi wa nyumba. (uk 13)
- Ni mvumilivu kwani anavumilia maisha ya umaskini hata bila kujiua baada ya kufutwa kazini.
- Ni mume kwani ni mume wake Nabaganzi.(uk 13, 81)

**<u>MAUDHUI YALIYOMO:</u>**

Maudhui ni jumla ya mambo, mawazo, mafunzo, maoni na ujumbe unaowasilishwa na mwandishi wa kazi ya kifasihi.

Katika tamthilia ya chema chajiuza, mwandishi Innocent Agume alishughulikia maudhui kadhaa, na baadhi ya hayo ni kama vile;

- **Mapenzi**: Mapenzi ni hali ya mvuto na upendo alionao mtu kwa mtu mwingine. Katika tamhilia hii ya chema chajiuza upendo huonekana kati ya Kwatampola na mkewe Kunihira (uk 27), Mzee Bahemuka na Bi-Shogora (23), Bakehena na Nabaganzi (uk 81), Bumaali na wake wake wawili yaani Bi-Machu na Bi-Akello (uk 116) (uk…)
- **Ujasiri**: Hii ni hali ya kutokuwa na uoga aukutoogopa kitu chochote kwamfano, katika tamthilia hii ya chema chajiuza ujasiri unaoneka pale Nabaganzi na Kunihira walipojivunia na kufanya kazi na wajenzi wanaume bila uoga. (uk 32, 90)

- **Utumishi**: Ni hali ya kufanyishwa kazi kwa malipo au kutolipwa. Katika tamthilia hii, Kwatampola anasema kwa kumjibu Bumaali ‘’ taja mtumishi wako yuko tayari kutimiza wajibu’’ (uk 12), Bakehena, Nabaganzi, Kunihira na wajenzi wengine ni watumishi. r
- **Uzazi**: Hii ni hali ya kuzaa. Kwamfano katika tamthilia hii ya chema chajiuza mwandishi Innocent anatuonyesha kwamba Kwatampola na Kunihira walimzaa Ben (uk 47), Bahemuka na Bi-Shogora walimzaa Kwatampola (uk 21), lubengula alimzaa Bumaali nk rejelea(uk 12)
- **Ndoa**: Ni mafanikio rasmi baina ya mwanamume na mwanamke ili waweze kuishi pamoja kama mke ne mume. Katika tamthilia hii ya chema chajiuza, ndoa inapatikana kati ya Bwana Kwatampola na Kunihira, Bumaali na wake wake wawili (uk 116, 113), Bakehena na Nabaganzi nakadhalika.
- **Wizi**: Ni tendo la kuchukua kitu kisicho chako bila ruhusa la mwenyewe. Kwamfano mwandishi anatuonyesha kwamba mitaimbwa, rangi na mabati yaliibwa huko katika uwanja wa ujenzi(uk 102) Pia, injinia Bakehena alimuiba Bumaali mwajiri wake na kisha akafutwa kazini. (uk 13) rejelea tena (uk 55)
- **Mabadiliko**: Ni hali ya kugeuka kwa mambo. Katika tamthilia hii, mwandishi Innocent anatuonyesha wahusika wengi ambao maisha yao yalibadilika kama vile Kwata kutoka umaskini kuwa mtajiri (uk 115), Bakehena alibadilika toka utajiri kuwa maskini alipofutwa kazini (uk 81).
- **Utajiri**: Ni hali ya kuwa na mali au fedha nyingi sana. Kwamfano tamthilia hii ya chema chajiuza inatuonyesha kwamba kabaila Bumaali ni mtajiri kwakuwa anamiliki nyumba nyingi na pia anampa kwata milioni thelathini za kununua vifaa vya kujenga ugo na kulipa vibarua (uk 13) Kwatampola ni mtajiri baada ya kupewa jumba la Nyamitanga (uk 115)
- **Umaskini** katika tamthilia hii ya chema chajiuza: Umaskini ni hali ya kutokuwa na hela au mali. Kwamfano tunaonyesha wahusika wengi ambao ni maskini kama vile Kwatampola alikuwa maskini kabla ya kuzawadiwa na jumba kwani tunaona alikuwa analala katika kiota kama ndege (**uk27**), Bakehena badaaye aligeuka kuwa maskini hadi kufika kiwango cha kutafuta kazi huko Fortportal (uk 13), Nabaganzi hadi kufika kufanya kazi ya ufagizi (uk 90), Kunihira anasema Ben ameenda kwa jirani kuona Runinga na huo huonesha umaskini. nk.
- **Ndoto**: Ni maono yanayotokea usingizini. Kwamfano katika tamthilia ya chema chajiuza, tunamuona Kwatampola aliota kuwa mtajiri halafu akawa (uk 02)

- **Utiifu**: Ni tabia ya adabu au nidhamu, hali tendo au uwezo wa kufuata amri au kutii. Kwamfano Kunihira anamtii mume wake Kwatampola, Kwatampola anamtii Bumaali kwani tunamuona anampa hata kutomuita jina bali humuita ''Mzee''
- **Uvumilivu**: Ni hali ya kuvumilia maisha magumu. Kwamfano katika tamthilia ya chema chajiuza , mwandishi Innocent anachora Nabaganzi kama mvumilivu kwakuwa anavumilia hali ya umaskini na kfanya kazi ya ufagizi baada ya mume wake kufutwa kazini (uk 13), kwatampola na mkewe wanavumilia maisha ya umaskini (uk 27) nk

- **Elimu**: Ni mafunzo yanayotolewa na jamii kwa watu ama darasani au pasipokuwa darasani. Kwamfano tunamuona Injinia wa tatu ni msomi (uk…), Ben anasoma(uk 09)nk
- **Utengano**: Ni hali au tendo la kuachana na kukaa mbalimbali na kitu kingine bila kushirikiana. Kwamfano katika tamthilia ya chema chajiuza, tunaona utengano kati ya Kwatampola na Mke wake Kunihira alipofanya talaka, Machu anatengana na familia yake na kuolewa kwa Bumaali (uk 47, 113)
- **Nyimbo**: Ni sauti zilizopangwa kimziki. kwamfano katika tamthilia ya chema chajiuza, mwandishi Agume Innocent anatuonyesha mziki unadundwa na mc.Bob King katika sherehe ya harusi ya kumuoa Bi-Machu (uk 111).
- **Utamaduni**: Hii ni mila, asili, jadi na desturi zinazofutwa na kundi la jamii Fulani. Kwamfano tunamuona Bumaali anasema ''kulingana na mila na desturi zetu, Kwatampola hatalajiwi kuwa katika kalamu hii'' (uk 113). Hii ni kwasababu katika tamthilia mwandishi anatuonyesha kwamba Kwata ni ami yake Machu.

**<u>MBINU ZA UANDISHI:</u>**

Mbinu au fani na uteuzi wa maneno na kuwekwa katika kazi za kifasihi ili kuifanya lugha iwe ya kuvutia na kupendeza.

Mwandishi wa tamthilia hii ya chema chajiuza Innocent Agume ametumia mbinu kadhaa kuvutisha na kupendesha kazi yake, na baadhi ya mbinu hizo ni kama;

- **Methali**: Ni misemo ya hekima yenye maana iliyofumbwa. Kwamfano Katika tamthilia hii, tunaona methali kama haraka haraka haina Baraka (uk 02), kila mbwa na siku yake (uk 13), hakuna siri ya watu wawili (uk 17), dawa ya moto ni moto (uk 49), akufanyia kwa dhiki ndiye rafiki (uk 43), mtenda mema hulipwa mema (uk 105).

- **Semi Na Nahau**: Ni fungu la maneno yanayotumika kutoa maana nyingiine badala ya ile ya maneno yaliyotumika. Semi hutumika kuficha maneno makali au kupamba lugha. Mwandishi katika tamthilia hii hutuonyesha semi kam vile vuta nikuvut (uk 21), siku ayami (uk 21), cha mtema kuni (uk 58), kata kauli (uk 14) nk.
- **Maswali Ya Balagha**: Haya ni maswali au masimulizi yasyohitaji majibu. Kwamfano katika tamthilia hii ya chema chajiuza mwandishi anatuonyesha maswali kama vile ‘’una nini ambacho ulininunulia nikisahau?’’ (uk 85), ‘’wamejigamba kama wewe, wakajuta badaaye?’’ (uk 85), ‘’jina lako sasa halina soko?’’ (uk 87) nk..
- **Takriri**: Hii ni mbinu ya kurudirudia neon au fungu la maneno ili kusisitiza ujumbe Fulani. Kwamfano katika tamthilia ya chema chajiuza tunaona urudiaji wa maneno kama vile, leo ni leo (uk 14), Kwata anasema ‘’kwa hizo hizo nitafanya kazi yako’’ (uk 14), wasiwasi (uk 13), nyumba ni nyumba bora imesimama (uk 30), dhiki ni dhiki hata iwe ndogo (uk 43), Ben Analia kwi kwi kwi, ‘’mama usiniache mama usiniache’’ (uk 47).
- **Tashibihi**: Hii ni mbinu ya lugha inayolinganisha vitu au hali mbili tofauti kwa kutumia maneno ya kulinganisha kama vile, kama, mithili ya, sawa na, nk. Na katika tamthilia tunaona mbinu ya tashibihi inajitokeza pale kwamfano ‘’tufe kama mtakatifu Stefano aliyekubali kifo cha kosa ambalo hakulifanya’’ (uk 4), Bumaali alimuita Kwatampola kwa kazi ngumu kama mawe (uk 12), amejenga kubwa kama dunia wamasaba ya Bugisu (uk 13), mjinga kama baba yako (uk 45), wanamziki ni kama mbwa (uk 108).
- **Kuchanganya Ndimi**: Hii ni hali ya kutumia maneno yasiyo ya kiswaahili katika lugha ya Kiswahili. Kwamfani katika tamthilia hii ya chema chajiuza kuna maneno kama radio west (uk 99), posho (uk 99), Balya hardware (uk 14), ok one two three (uk 108), Mbarara Regional Referal (uk 116).

- **Utohozi**: Hii ni mbinu ya kuwasilisha maneno ya lugha nyingine yatamkwe katika Kiswahili. Kwamfno mwandishi anatumia maneno kama hospitalini (uk 115), dereva (uk 116), korasi, sinema nk
- **Chuku**: Hii ni kutilia chumvi ili kusisitiza ujumbe Fulani. Kwamfano katika tamthilia hii ya chema chajiuza, mwandishi anatuonyesha chuku kama Bumaali alipomwambia Kwata ‘’nakuamini kushinda ninavyojiamini’’ (uk 13), shogora anasema ‘’maji yamepita kiwango cha baridi, sijabakiza hata jino moja’’ (uk 24)
- **Majazi**: Hii ni mbinu ambayo mtunzi wa akzi ya fasihi hutumia kufananisha tabia za wahusika na majina yao halisi. Kwamfano katika tamthilia mwandishi alitumia majina kama ‘’Bakehena’’ maana ya kwamba mjifanyia mabaya. Tena kabaila Bumaalai kwakuwa alikuwa mjajiri sana. Kwatampola kwa maana ya kutenda mambo yake kiupole bila kuruka ruka.
- **Taswira**: Hii ni mbinu inayomfanya msomaji kupiga picha ubongoni. Kwamfano (uk 115) kwatampola tunamuona anapewa zawadi la jumba.
- **Uzungumzaji Nafsi**: Hii ni mbinu inayomhusu mhusika anapojizungmzia au kwa kuongea au kuwaza bila kukusudia kusikika na yeyote. Kwamfano tunamuona Kwatampola katika tamthilia anazungmza mwenyewe baada ya kupewa pesa za kujenga ugo (uk 14).
- **Hotuba**: Hii ni mbinu inayotoa mazungmuzo yanayohusu jambo maalumu, kwamfano tunamuona Bi-Akello anatoa hotuba (uk 113), hotuba ya Bumaali (uk 112).
- **Kisengere Nyuma**: Hii ni mbinu ya Sanaa ambayo mwandishi hutumia kusimulia mambo yaliyotokea huko nyuma, kwamfano Bumaali anamuelezea kwata jinsi babake lubengula alivyopenda mchezo huo wa kuoa wengi (uk 12).
- **Taharuki**: Hii ni mbinu inayoibuka baada ya msomaji kusoma na kubaki na hamu ya kuendelea kusoma. Kwamfno kunihira anapotoka shoti na wakamhudumia pale alipoanguka na kumpeleka hospitalini (uk 115), taharuki inawabakia watu wakijiuliza je, alipofika huko hospitalini palitokea nini? Nakadhalika.
- **Mazungumzo**: Ni majadiliano kati ya watu wawili au Zaidi kuhusu jambo Fulani, kwamfano kuanzia ukurasa wa kwanza hadi ya mwisho ni mazungmzo kwani kuna maogezi kila onyesho.
- **Tasihishi**: Hii ni mbinu ya kupatia kitu kisicho na uhai kuwa na sifa za kiumbe mwenye uhai. Kwamfano Injinia wa kwanza anasema ‘’mawingu yanapiga makofi kwa furaha zako’’

(uk 102) Pia, Bakehena anasema ''jina lako litaanza kusafiri mawinguni kama ndege'' (uk 75).

- **Nyimbo**: Ni mbinu ya kutumia nyimbo katika kazi ya kifasihi kufikisha ujumbe kwa hadhira, kwamfano kuna nyimbo katika sherehe za harusi unaoogozwa na Mc-Bob King Mfawidhi (uk 111, 110).

<u>**N.B**</u>: ***Ikumbukwe kwamba mwongozo huu haubebi yote namna inavyojitokeza katika mchezo, kwa hivyo inakubidi wewe kama mtumiaji kusoma mchezo kwanza na kasha ukasome mwongozo kukusaidia kuelewa vipengele mbalimbali vinavyopatikana na ambavyo vimeangaliwa hapa ndani. Asante!!!***